JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA KUMI NA NNE

06 MEI, 2016

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA KUMI NA NNE – TAREHE 06 MEI, 2016

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji

juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

## II. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**110. MHESHIMIWA VEDASTO EDGAR NG'OMBALE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Moja ya matukio makubwa ya kihistoria katika nchi yetu ni vita ya Majimaji iliyopiganwa kati ya mwaka 1905 – 1907 kati ya Watanganyika na Wajerumani; pamoja na kufahamu kwamba vita hivyo vilienea katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, lakini vilianza katika Kijiji cha Nandete Wilaya ya Kilwa; Serikali inaonyesha jitihada mbalimbali ya kuienzi historia hiyo, ikiwa ni pamoja na kujenga mnara katika Kijiji hicho:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara ya kutoka Njianne hadi Nandete kwa kiwango cha lami ili kulifanya eneo hilo la kihistoria kufikiwa kwa urahisi na kuliongezea umaarufu kwa kutembelewa na watalii hususani wa kutoka Ujerumani jambo ambalo litaiongezea mapato Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa na Taifa kwa ujumla.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

### 111. MHESHIMIWA DOTO MASHAKA BITEKO (BUKOMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, kwa nini Serikali inachukua muda mrefu sana kurekebisha mishahara ya Walimu baada ya kupandishwa vyeo.

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

### 112. MHESHIMIWA KHAMIS MTUMWA ALI (KIWENGWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inafanya ukaguzi katika Taasisi za Tanzania Bara na Zanzibar:-

Je, Ofisi hii inashirikiana vipi wakati wa kufanya ukaguzi wa Taasisi za Muungano na Ofisi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Zanzibar.

**113. MHESHIMIWA UPENDO FURAHA PENEZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kupunguza misamaha ya kodi kufikia asilimia moja (1%) ya GDP.

## WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

**114. MHESHIMIWA TASKA RESTUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Mkoa wa Katavi ni miongoni mwa Mikoa ambayo haina Kiwanda hata kimoja:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani kujenga viwanda katika Mkoa wa Katavi;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa mafunzo ya Ujasiliamali kwa Wanawake na Vijana wa Mkoa huo.

**115. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Ujenzi wa masoko ya kimataifa yaliyokuwa yakijengwa huko Nkwenda na Murongo umesimama kwa muda mrefu sana na Wananchi wa Wilaya ya Kyerwa walitegemea masoko hayo kwa ajili ya kuuzia mazao yao mbalimbali:-

Je, ni nini kimesababisha kusitishwa kwa ujenzi wa masoko hayo, na ni lini sasa ujenzi utafufuliwa na kukamilishwa ili kutoa fursa za kufanya biashara na kwa majirani zetu pia.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**116. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Wananchi wa Jimbo la Nanyamba kwa muda mrefu wamekuwa wakipata shida ya ukosefu wa maji safi na salama:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Wananchi hao wanapata maji safi na salama.

**117. MHESHIMIWA LIVINGSTONE JOSEPH LUSINDE (MTERA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Mradi wa maji wa Kijiji cha Manzase ulishalipiwa nusu ya gharama za Mradi na Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne.

(a) Je, Serikali ya Awamu ya Tano ina mpango gani kuukamilisha ili Wananchi wa Kijiji hicho wapate huduma ya Maji Safi na Salama;

(b) Kijiji cha Chinoje kilipata Mradi wa Maji wa World Bank na kuchimbiwa visima kumi (10) lakini maji hayakupatikana. Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo la maji katika kijiji hicho.

**WIZARA YA KAZI KATIBA NA SHERIA:**

**118. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM MALEMBEKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Matukio ya kubakwa na ulawiti kwa watoto nchini yamekuwa yakijirudia mara kwa mara na watuhumiwa walio wengi huachiwa au humalizana na wazazi wa waathirika kifamilia:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa kesi hizo hazimalizwi kifamilia;

(b) Je, ni mkakati gani umewekwa ili kuhakikisha kuwa watuhumiwa hao wanapopatikana na hatia wapewe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine wenye nia mbaya;

(c) Je, watoto waliopatwa na matukio hayo wamewekewa mazingira gani ili kuwaondoshea msongo wa mawazo na kuendelea na elimu bila kubughudhiwa na wenzao.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**119. MHESHIMIWA NJALU DAUDI SILANGA (ITILIMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-Sekta ya afya hutenga fedha za mfuko wa pamoja (HSBF) kwa ajili ya kununua dawa, vifaa tiba n.k.:-

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuboresha mfumo wa manunuzi ili kupunguza mlolongo mrefu wa manunuzi uliopo sasa

wa Halmashauri kutoa fedha kisha kusubiri mpaka MSD itafute mzabuni mwingine;

(b) Mgao unaotolewa kutoka MSD kwenda vituoni ni kwa vituo vyenye fedha tu; Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa vituo vyote vinapata dawa kwa wakati ili kuhudumia Wananchi wake.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**DODOMA** **DKT. T. D. KASHILILAH**
**06 MEI, 2016** **KATIBU WA BUNGE**